BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA SABA

Kikao cha Pili – Tarehe 28 Aprili, 2022
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

I. TAARIFA YA SPIKA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mwaka 2022/2023.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa Mwaka 2022/2023.

III. MASWALI:

Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

26. MHESHIMIWA HABIBU ALI MUHAMED (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inapata mgao wa asilimia ishirini na moja (21%) ya ajira kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Je, ni vijana wangapi walioajiriwa katika jeshi la Polisi na Uhamiaji kwa mwaka 2021 kwa upande wa Zanzibar.

Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

34. MHESHIMIWA YAHYA RASHID ABDULLA (Jimbo la Kwahani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Katika kutimiza miaka 50 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar Serikali ilianzisha Makumbusho ya Mapinduzi na kujenga Mnara katika maeneo ya Kisonge.

(a) Je, ni sababu gani zilizopelekea makumbusho hayo hadi sasa kuwa bado hayajakamilika.

(b) Je, jengo la kumbukumbu ya Mapinduzi la Kisonge linatumika kwa shughuli gani.

(c) Ni lini makumbusho hayo yatakamilika na kutumika kama ilivyotarajiwa.

Wizara ya Afya:

2. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya.

Katika miezi ya hivi karibuni kulijitokeza sakata la uingizaji wa kitoweo cha kuku ambao tayari wameshachinjwa hali ambayo ilipelekea Mkuu wa Wilaya ya Magharibi "B" kuzuia uingizaji wa bidhaa hiyo kwa hofu ya kuingiza maradhi nchini.

(a) Je, Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi (ZFDA) wana

mpango gani wa kupiga marufuku uingizaji wa bidhaa hiyo.

(b) Je, ni Wizara gani yenye mamlaka ya kuingiza bidhaa hizo.

(c) Je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu wa taasisi zote husika kukaa pamoja ili kumaliza tatizo hilo.

75. MHESHIMIWA MOHAMMED MGAZA JECHA (Jimbo la Mtambile) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Serikali ina nia njema ya kujenga hospitali za Wilaya katika maeneo tofauti ndani ya visiwa vyetu vya Unguja na Pemba ili ziweze kuwahudumia kikamilifu wananchi wetu.

Je, hospitali hizo zitakuwa na vifaa vya kutosha kuepusha yale yaliyotokea ya kupoteza mtoto kwa uzembe wa daktari.

<u>Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:</u>

60 MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kwa kawaida barabara haziwezi kujengwa bila kupata mali ghafi (*raw materials*) kama vile mawe na kokoto. Hata hivyo, Serikali imekuwa na tabia ya kuzisahau barabara muhimu zinakotoka mali ghafi hizo kama vile barabara ya Mjini Wingwi, barabara ya Muambe, barabara ya Vitongoji, na barabara ya Kibele.

(a) Je, ni sababu zipi zilizopelekea kutoziimarisha barabara hizo.

(b) Je, ni lini Serikali itazijenga barabara hizo.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:

73. MHESHIMIWA ABDALLA ABAS WADI (Jimbo la Nungwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kutokana na mabadiliko ya elimu ya msingi kutoka darasa la sita kwenda la saba ambapo mabadiliko hayo yanaweza kupelekea changamoto ya matokeo yasiyo mazuri hasa kwa upande wa skuli za shamba, miongoni mwa skuli hizo ni skuli ya Nungwi kutokana na kuwepo kwa uhaba wa walimu.

(a) Je, Serikali ni lini itaajiri walimu ili kuihami hali hali hii.

(b) Je, ni utaratibu gani unaotumika kuwapa kipaumbele cha ajira walimu waliokwishajitolea kwa muda mrefu ili kuweza kuthamini mchango wao.

(c) Je, Serikali inafahamu kwamba katika mchakato wa ajira hizo yanachukuliwa majina kwa kujuana.

Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

22. MHESHIMIWA HABIBU ALI MUHAMED (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Kumekuwa na malalamiko mengi ya wakulima wa karafuu ambao mashamba yao yamekodishwa na Serikali, kufuatia agizo la Serikali la wakulima hao kurejeshewa fedha zao.

Je, ni sababu zipi zilizopelekea mpaka leo wakulima hao kutopatiwa malipo yao.

Wizara ya Uchumi wa Buluu:

58. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Ni jambo la kupongezwa kwamba Serikali imeonyesha dhamira njema katika kuwaendeleza wakulima wa mwani nchini. Hata hivyo, upatikanaji wa vifaa au nyenzo za ukulima huo ni changamoto.

(a) Je, Serikali imeweka utaratibu gani katika uingizaji na uuzaji wa vifaa na nyenzo za ukulima wa mwani.

(b) Je, ni lini Serikali itafungua maduka maalumu ya nyenzo au vifaa hivyo ili wakulima hao waweze kupatiwa unafuu wa bei au mikopo ya nyenzo na vifaa vya mwani.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Kwamba Baraza hili liingie katika Kamati ili kujadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi kwa mwaka 2022/2023.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

Kwamba Baraza hili liingie katika Kamati ili kujadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mwaka 2022/2023.

Zanzibar,
28 Aprili, 2022.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA